Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 7, Issue 3

15th Rabee ul-Awwal 1432

18th February, 2011

SABABU YA KUFUATA NJIA YA SALAF

Mtayarishi: Sheikh Saleem Bin 'Eid al-Hilaalee (حفظه الله)

Kwa hakika, wanaojishugulisha katika uwanja wa Da'wa ya Uislamu wameongezeka idadi yao, na wale wanaoelekeza huduma zao kwa vijana wa "Mwamko wa Ki-islamu" ni wengi. Watu wote hawa wanaojishugulisha kwa juhudi kubwa, mpaka wanakuwa ta'bani ili hali ya kimaisha ya Uislamu irudi upya. Na kati ya mifuriko hii na misukosuko ya bahari, utakuta mapote ya wazee na vijana. Amma kuhusu wazee, utawona wao wamejikinai warudi majumbani mwao watizame maisha yao. Lakini kuhusu vijana, wanajifunga vibobwe na kuwahamasisha farasi wao kwa kuwapiga mateke. Ingawaje, mapote yote haya yamechanganyikiwa na yako kwenye balaa kubwa. Kwahivyo inabidi mawazo ya Manhaj Ya Salafee yawasilishwe kwao kuhusiana na uhuishaji wa uongofu wa mfumo wa maisha ya ki-Islamu juu ya misingi ya Utume:

Kwa kweli, (1) ***KUUTAKASA*** Uislamu kutokamana na yaliozushwa, juu ya Imani, hukumu na desturi ili upate kwa umakinifu kurudi kwenye hali yake ya utakaso na ubainifu kama ulivyo teremshwa kwa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Na (2) ***KUWAELIMISHA*** vizazi vya Waislamu juu ya Uislamu swafi (uliotakata) na kuwalea juu ya misingi ya Imaani (iliyo wima) na vitendo thabiti. Hii ndio njia ya Da'wa ya Salafi na pote lenye ushindi katika kuleta mabadiliko:

KWANZA:

Ni kwanini basi iwe Manhaj Ya Salafi?

Kwa kila Muislamu anaependelea kufuzu na atazame njia iliyo bora ya kimaisha ili apate ne'ema katika maisha ya hapa duniani na kesho akhera, ni lazima akifahamu kitabu cha Allaah (سبحانه وتعالى) na Sunnahh zilizo swaheeh za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kulingana na walivyofahamu wabora wa viumbe. Nao ni Maswahaba, *ma-Taabi'in* (wafuasi wao) na wale waliowafuata wao kwa wema hadi siku ya malipo. Hii ni kwa sababu haimkiniki kudhaniwa, yakwamba kuna mwenendo, ufahamu au njia iliyo swaheeh au iliyo sawa kuliko ufahamu na njia ya *Salafu-us-Salih* (wema waliotutangulia). Na pia ni kwa sababu sehemu ya mwisho ya Umma huu hautorekebishika, isipokuwa kwa kile kilichourekebisha sehemu yake (Umma huu) ya kwanza .

Na kwa hakika, iwapo mtu yeyote akifanya uchunguzi na upelelezi juu ya ushahidi utokao kwenye Qur'an, Sunnahh, muafaka wa wanavyuoni na makadirio ya kiujuzi ya ki-dini, atona yakwamba ni wajibu kuifahamu Qur'an na Sunnahh kwa mwangaza wa njia ya *Salaf-us-Saalih*. Hii ni kwa sababu huu ndio ufahamu ambao uthabiti na uswaheeh wake umekubaliwa katika karne nyingi zilizoandamana. Kwa hivyo kutokamana na hayo, hairuhusiwi kwa mtu yeyote, bila ya kujali cheo chake, kuwa na ufahamu kinyume na walivyofahamu (mambo hayo) ma-salaf.

Na yeyote atakaekengeuka na kuuridhia uzushi wa *khalaf* (Waislamu mamboleo) uliozungukwa na mambo ya hatari yasokuwa na upande ulio na usalama-na matokeo yake ya kugawanya Waislamu yanajulikana vyema bila ya ubishi, kama ilivyo matokeo yake katika kuufarakanisha Umoja unavyofahamika na wala hauwezi kupuuzwa - basi huyu ni mtu alojenga msingi wa nyumba yake pambizoni mwa jabali lililokurubia kuporomoka wakati wowote. Mbele yako ni ubainifu wa hoja hii ulostawi juu ya dalili na ushahidi kamili.

1. Allaah, Alietukuka, amesema: **"Na wale waliotangulia wakawa wakwanza katika (Uislamu)- Muhajiri na Ansari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri - Allaah atawapa radhi, nao wamridhie (Allaah kwa hayo mazuri atakayowapa) na amewaandalia mabustani yapitayo mito mbele yake, wakakae huko milele. Huku ndiko kufuzu kukubwa.** [Surat at-Tawba:100].

Nukta ya ushahidi iliyopatikana kutoka kwenye aya hii ni kwamba **"Mola wa Walimwengu"** amewasifu wale waliofuata **"Bora wa Walimwengu".** Kutokana na hayo itafahamika hapa kuwa ikiwa "bora wa walimwengu" wakisema jambo, basi mtu huwafuata wao kwa hilo na inampasa mtu huyo asifiwe kwa kuwafuata na vile vile astahiki radhi za Allaah. Na iwapo hakuna tofauti baina ya kuwaandama wao au kuwaandama wasokuwa wao, basi hapana atakaestahiki sifa na radhi. "Bora ya walimwengu" ni Maswahaba na wale walowafuata wao kwa wema, kutokana na *Nass'* ya Qur'an: **"Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema**

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

SABABU YA KUFUATA NJIA YA SALAF 1 - 4

SABABU YA KUFUATA NJIA YA SALAF

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

wa viumbe." [Surat al-Bayyina]

2. Akasema Allaah: **"Nyinyi ndio Umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (Ulimwenguni)-mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamuamini Allaah."** [Surat Aali 'Imraan :110]

NUKTA YA USHAHIDI: Allaah **(** سبحانه وتعالى**)** ameuthibitisha ubora wao juu ya Mataifa yaliyosalia. Imebidi kupatikana hali hiyo kwa kutokamana na misimamo na uvumilivu wao katika dini, juu ya hali yoyote kwani hawakupotoka kutoka kwenye uongofu uliowazi. Kwahivyo Allaah anashuhudia yakwamba wao wanawaamrisha (wengine) kuhusu kila jema na wanawakataza (wengine) kutoka kwenye kila ovu, wakitarajia malipo kwa imani iliothabiti. Hali hii inashurutisha yakwamba ufahamu wao (wa dini) ni chanzo cha maamrisho na kujitegemeza kwa wale watakaokuja baada yao hadi siku ya malipo. Na ikiwa hivyo sivyo, basi haitokuwa sawa kusema yakwamba wao wanaamrisha mema na kukataza maovu, hebu tafakari na uzingatie.

Iwapo itasemwa: "Aya hii ni yenye kujumlisha na inahusu Taifa zima (la Waislamu) bila ya kuwa makhsusi kwa kizazi cha Maswahaba peke yao mbali na wale walokuja baada yao)". Basi Mimi nasema: "Wao ndiwo waliokusudiwa mwanzo zaidi (kwenye hiyo aya). Na 'wale waliowafuata kwa mwendo mzuri' hawaingi kwenye maana ya aya isipokuwa kwa njia ya vipimo vya kulinganisha au ushahidi mwengine, kama iliyokuwa kwenye dalili ya kwanza (iliyotajwa hapo juu)."

Na juu ya makubaliano kuhusu kusema kuwa aya hiyo inazungumzia kwa ujumla - basi hilo ndilo lilo sawa- kisha Maswahaba ndiwo wa kwanza kuingia ndani ya kiini cha maneno yaliyokusudiwa. Hii ni kwa sababu wao ndiwo wa kwanza kujifunza na kuuchukuwa ujumbe kutoka kwa Mtume **(** صلى الله عليه وسلم**)**, moja kwa moja, bila ya kuwepo mjumbe yoyote (baina yao na yeye, Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)**). Nao ndiwo wa kwanza kuuhudumikia uteremsho (wahyi) na kuutendea kazi.

Wanakuwa wao ni aula zaidi katika kuingia kwenye maana ya aya hii kwani hapana aliepambika na tabia ambazo Allaah alizowasifu nazo, kwenye hali iliyo bora ya ukamilifu, isipokuwa wao. Kwahivyo makubaliano ya sifa na mapambo ni ushuhuda unaoashiria yakwamba wao wana haki zaidi kuliko wengine kuhusu sifa hii. Hii ndiyo sababu:

3. Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** amesema: *"Bora ya watu ni wa karne yangu, kisha ni wale walokuja baada yao na kisha ni wale walokuja baada yao. Kisha kutakuja watu ambao mmoja wao (itambidi) awasilishe ushahidi wake kwa kula kiapo. Na kiapo chake kitakuwa ndio ushuhuda wake".*

Jee, ni kwa ajili gani ubora wa Maswahaba umethibitishawa hapa, unadhani ni kwa rangi zao, miili yao, utajiri wao au majumba yao?

[Hadith Mutawaatir kama ilivyotajwa na Al-Haafidh Ibn Hajar katika Al-Isaaba (1/12) Na As-suyuti, Al-manaawi na Al-kanaani wamekubali].

Hapana mtu yoyote mwenye fahamu zake njema, mwenye ujuzi wa Qur'an na Sunnahh zilizo swaheeh, atakae kushuku chochote miongoni mwa hayo yalotajwa, kwamba sio makusudio. Na hii ndio sababu, Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** akasema: *"Kwa hakika Allaah hatazami sura zenu na utajiri wenu. Lakini badala yake antazama nyoyo zetu na vitendo vyenu."*

[Imepokewa na Muslim (16/121 ya an-Nawawi)].

Na pia hii ni kwa sababu hali ya usawa inyoyakinisha ubora wa mtu katika Uislamu ni taqwaa ya nyoyo na vitendo vyema, kulingana na maneno ya Allaah **(** سبحانه وتعالى**)**: **"Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allaah ni yule mwenye Taqwaa zaidi."** [surat al-hujurat: 13].

Na Allaah kwa kweli ametazama ndani ya nyoyo za Maswahaba **(**رضي الله عنهم**)** na akaziona kuwa bora miongoni mwa nyoyo za waja wake baada ya moyo wa Muhammad **(**صلى الله عليه وسلم**)** . 'Abdullah Ibn Mas'ud **(**رضي الله عنه**)** akasema: **"Kwa hakika Allaah ameziangalia nyoyo za waja (Wake) na akaona yakwamba moyo wa Muhammad (**صلى الله عليه وسلم**) ndio bora ya nyoyo za waja, kwahivyo akamchagua yeye kwa ajili yake mwenyewe na akamtumiliza na ujumbe wake. Kisha akaangalia ndani ya nyoyo za watumishi nyuma ya moyo wa Muhammad (**صلى الله عليه وسلم**) na akaziona nyoyo za Maswahaba kuwa ni bora za nyoyo za watumishi (Wake). Basi akawafanya kuwa ni wasaidizi wa Mtume Wake (**صلى الله عليه وسلم**), kupigania dini yake."** [Hadith Mawquf (hayo ni matamshi ya Swahaba tu) yenye Silsila nzuri. Imepokewa na Imaam Ahmad (1/3/9) na wengineo.]

Allaah akawapa ilimu na ufahamu ambao hata wale walokuja baada yao hawakuufikia. Ikapokewa na Abu Juhaifa kuwa alisema: "Nilisema kumwambia 'Ali: 'Je una kitabu chochote wewe?' Akasema: La Isipokuwa kitabu cha Allaah, au ufahamu ambao mtu Muislamu aliopewa au kilicho hapa chini (andikwa) kwenye huu ukurasa.'" [Imepokewa na Imaam al-Bukhari, tazama (1/204) ya Al-Fat-h]

Kutokana na msingi huu, inakuwa wazi yakwamba ubora ulosifiwa kwenye maneno ya Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)**, hapana shaka ni ubora katika ufahamu na mwenendo. Kwahivyo, ufahamu wa Maswahaba wa Qur'an na Sunnahh ni chanzo cha maamrisho na muelekeo kwa wale watakaokuja baada yao hadi sehemu ya mwisho ya Taifa hili. Kitu kinacho- fafanua zaidi jambo hili ni:

4. Maneno ya Allaah **(**سبحانه وتعالى**)**: **"Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora (muadilifu) ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu."** [Surat-al-Baqara:143]

Allaah, Mwenye Nguvu, na Aliye Mtukufu Amewafanya wao kuwa bora na waaminifu miongoni mwa watu. Hivyo basi ni Taifa lilo bora na wakweli zaidi kwenye maneno yao, vitendo na mahitaji. Kwa ajili hii, wanastahiki kuwa mashahidi juu ya watu. Hii ndiyo sababu Allaah amewataja kwa uzuri, akawanyanyuwa daraja zao akawasifu na kuwapokea kwa mapendeleo mazuri.

Shahidi ambae ushahidi wake umekubaliwa na Allaah ni yule ambae anaeshuhudia kwa ilimu na ukweli. Mtu

SABABU YA KUFUATA NJIA YA SALAF

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

huyu anasimulia kwa ukweli akiegemeza ushahidi wake juu ya ilimu yake. Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **"Ila wale wanaoikiri hii haki, wakaijua."** [Surat az-Zukhruf: 86]

Sasa iwapo ushahidi wao unakubaliwa na Allaah, basi hapana shaka yakwamba ufahamu wao wa dini ni chanzo cha maamrisho na muelekeo kwa wale watakaokuja baada yao. Na lau kama si hivyo, basi kiapo chao cha ushahidi hakingelithibitishwa. Na dalili yake imepasishwa na aya pasi na mushkili wowote. Zaidi ni kwamba, Taifa hili (la Waislamu) halijakubali uswaheeh wa zama zozote bila ya pingamizi, isipokuwa kwa zama za Maswahaba. Kwani, Ahl-us-Sunnahh wal Jamaa'ah, kutoka katika wafuasi wa Salaf na Ahl-ul-Hadeeth, wote wameidhinisha ukweli na uaminifu wa Maswahaba katika hali zisokuwa makhsusi na bila ya kizuizi chochote. Wao wamezikubali kutoka kwao riwaya zao na ilimu yao pasi na kuondoa au kuacha chochote. Jambo hili ni kinyume cha wale wasokuwa Maswahaba, kwani hawakuwaidhinisha (hawa watu wengine) kuwa ni wakweli na waaminifu, isipokuwa wale ambao uhodari wao (katika kusimulia) umethibitishwa na uaminifu wao umekubalika. Na watu hawakupewa mambo haya mawili mpaka waandame njia ya Maswahaba, Allaah (رضي الله عنهم).

Kwahivyo imethubutu kwa haya yakwamba ufahamu wa Maswahaba ndio chanzo cha maamrisho na muelekeo kwa wasokuwa wao, tunapo yaelekea maandishi ya Qur'an na Sunnah. Hii ndio sababu Allaah, Aliekamilika, alivyotuamrisha tufuate njia yao:

5. Amesema Allaah : **"Shika njia ya wale wanaoelekea kwangu na kutubia ."** [Surat LUQMAN:15]

Kila mmoja wa Maswahaba alielekea kwa Allaah na kutubia. Allaah nae Akawaongoza kwenye uzuri wa kwenye mazungumzo yao na wema wa vitendo juu ya dalili ya maneno ya Allaah yasemayo: **"Wakafuata zile zilizo njema (Qur'an). Hao ndio aliowaongoa Allaah. Na hao ndio wenye akili".**[Surat az-Zumar:17-18]

Kwahivyo ni wajib kufuata njia yao kuhusu kuifahamu dini ya Allaah kulingana na kitabu chake na Sunnah. Kwa sababu hii, Allaah amewaonya vikali wenye kufuata njia isiokuwa yao na Moto wa Jahannam-napo ni mahali pabaya sana pa mtu kurudia.

6. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya waumini, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamwingiza katika Jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia!"**[Surat an Nisaa (4):115]

NUKTA YA USHAHIDI: Allaah ametoa onyo kali kwa kufuata njia isokuwa ya waumini. Hivyo basi, hii inaashiria yakwamba kuifuata njia yao kwenye kuifahamu Dini ni wajibu. Na kwenda kinyume chake ni upotofu.

7. Abu Musa-Al-Ash'ari akatuhadithia: **"Tuliswali swala ya maghrib pamoja na Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) kisha tukasema: Hebu tukaeni na tusubiri ili tupate kuswali swala ya 'ishaa pamoja nae (pia). Kwahivyo tukakaa hapo kisha yeye (صلى الله عليه وسلم) akatutokea sisi na akasema : 'Ni jambo gani lilowawaeka nyie hapa?'Tukasema: 'Ewe Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم), sisi tuliswali na wewe kisha tukajiambia wenyewe: Hebu tukaeni na tusubiri ili tupate kuswali swala ya 'ishaa pamoja na wewe! Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Mumefanya jambo zuri" au mumefanya kitendo kizuri.' Kisha akanyanyua kichwa chake mbinguni mara kwa mara-huku akisema: 'Nyota ni mlinzi wa mbingu. Kwahivyo zinapo-ondoka nyota, shuguli za mbinguni huwa zimekamilika. Na mimi ni mlinzi wa Maswahaba zangu, na Maswahaba zangu ni walinzi wa Taifa langu, kwahivyo wanapoondoka Maswahaba zangu, basi Taifa langu litapata kile walichoahidiwa."** [Imepokewa na Muslim (16/82 ya An-Nawawi)]

Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameufanya uhusiano wa Maswahaba zake na wale waliokuja baada yao kutoka kwenye Taifa la Waislamu kama uhusiano wake Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake na kama uhusiano wa Nyota na Mbingu. Ni jambo linalojulikana wazi kuwa ulinganizi huu wa ki-Utume unawasilisha kuandama ufahamu wa Maswahaba ili Umma urudi nyuma huko kwa Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) Sababu ni kwamba yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiye aliyekuwa akiifafanua Qur'an na Maswahaba zake ndiwo waliouwasilisha ufafanuzi huo kwa Umma.

Na vile vile, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hazungumzi kwa mapendeleo yake, bali huo ni ukweli mtupu na uongofu utokao kwake. Na Maswahaba zake ni waaminifu; hawakuzungumza isipokuwa kwa uaminifu na hawakufanya jambo lolote isipokuwa kwa ukweli. Pia Allaah akazifanya nyota kuwa kama vimondo, vinavyowapiga Mashetani wanapojaribu kuiba minon'gono (ya wahyi kutoka mbinguni). Akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Bila shaka sisi tumeipamba Mbingu ya (daraja ya) karibu kwa pambo la Nyota. Na kuilinda na kila shetani 'asi. Wasiweze kusikiliza(yanayosemwa na hao) viumbe watukufu (Malaika); na wanafukuzwa huko kila upande kwa hizaya; na wanayo adhabu (inayowazuia kufika huko) inayodumu kwao. Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo hivi (katika maneno yanayosemwa huko); mara kikamfuata kimondo (kijinga cha moto) king'aracho (kikamuangamizilia mbali).** [Surat as-Saafaat:6-10]

Na Akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na kwa hakika Tumeipamba Mbingu ya (daraja ya) karibu hii kwa mataa, na tumeyafanya ili kuwapigia mashetani na tumewawekea tayari adhabu ya moto uwakao (kwa nguvu)**[Surah Al-Mulk:5].

Kadhalika, Maswahaba nao ni pambo la Taifa hili kwa upande wa ufahamu, ilimu na vitendo. Na huduma yao (pia) ni kama kimondo na dharuba dhidi ya tafsiri iliyo ba'til ya wajinga, uwongo wa wazushi na upotofu wa wenye kupindukia mipaka.

Na vile vile, Nyota ni miangaza kwa wakaazi wa kwenye ardhi hii inayowaongoza kwayo, katika nyakati za giza la ardhi na bahari. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na (ameziweka) alama nyengine. Na kwa nyota (pia) wao (wanaadamu) wanafuata njia".** [Surat an-Nahl:16]

Na akasema: **"Na yeye ndiye aliekuumbieni nyota ili mwongoke kwazo katika vizazi vya Bara na Bahari."**[Surat al-An'aam:97]

Lengo la kuwafuata Maswahaba ni kwa min-ajil ya kujiokoa kutoka kwenye giza la mapendelewa ya nafsi

SABABU YA KUFUATA NJIA YA SALAF

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

(*hawaa*) na shaka. Hivyobasi, yoyote atakaeupa nyongo ufahamu wao, katika kuhadaika kwake, anajizamisha mwenyewe kwenye giza- tabaka juu ya tabaka- kiasi cha kwamba anapouchomoza nje mkono wake hushindwa hata kuuona. Kwa kupitia ufahamu wa Maswahaba, Qur'an na Sunnah zinakuwa ni ngome dhidi ya Mashetani miongoni mwa watu na Majini - wale wanaotafuta uharibifu na maana zake za ndani zilofichamana ili kupotoa maana zilizokusudiwa na Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم). Utahisi yakwamba ufahamu wa Maswahaba ni ngome dhidi ya uovu na vinavyosababisha uovu huo. Lau kama ufahamu wao si chanzo cha maamrisho na kujitegemeza kwa wale watakaokuja baada yao, basi ufahamu wa wale walokuja baada yao ndio ungelikuwa ni ulinzi wa Maswahaba na pia ngome yao na jambo hili haliwezekani.

Na iwapo upambanuzi huu na himaya-zenye kujiambatanisha na Qur'an na Sunnah swaheeh kulingana na ufahamu wa Salaf-As-Saalih- zimekataliwa, basi Muislamu atapotoshwa kutoka kwenye njia ya sawa. Na atakuwa kinyang'anyiro cha mapote na vyama vilivyopotoka kutoka kwenye njia iliyonyoka. Hii imetokamana na majaribio mengi ya hila za uovo za jinsi ya kuzielewa Qur'an na Sunnah, kama vile hila za Mu'tazila, Murji'a Jahmiyya, Shi'ah, Soofiyya, Khawaarij, Baatiniyyah na wengine wasokuwa wao. Kwahivyo kipambanuzi hapana budi kiwepo. Na mtu akisema: Hapana shaka yakwamba ufahamu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake ndio njia au mfumo ambao hauwezi kukurubiwa na uwongo, ikiwa ni kwa mbele au nyuma yake.

Lakini, ni nini dalili eti Manhaj Ya Salaf ndiwo ufahamu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake?"

Mimi nasema: "Jawabu inapatikana kutoka kwenye njia mbili zilizowazi.

1) Mifano yalotajwa hapo mbeleni yalikuja baada ya kipindi cha Utume na kipindi cha Makhalifa wema. Na yule alotangulia (alokuja mwanzo) hawezi kujisifu kwa atakaekuja baadae (alokuja baadae), lakini jambo hilo ni kinyume chake. Kwahivyo imedhihirika yakuwa pote lolote lisiloandama njia hizo wala lisilofuata mapote hayo, ni lile lililobakia juu ya hali yake ya asili.

(2) Hatuoni yoyote miongoni mwa mapote ya Umma wa ki-Islamu aliye kwenye msimamo unaolingana na Maswahaba isipokuwa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*, kama wafuasi wa *Salaf-us-Saalih* na *Ahlul-Hadeeth* mbali na baadhi ya mapote.

Amma kuhusu Mu'tazila, ni vipi wao watafanana na Maswahaba ikiwa viongozi wao wanawasuta (kuwalaumu) na kuwasingizia Maswahaba walio bora, kuwaondoshea uaminifu wao na mategemeo, na kuwapa sifa za upotofu? Hiyo ndio hali ilivyotokea kwa *Waasil Ibn 'Ataa'* alisema: "Ikiwa 'Ali , Talha na Zubair watatoa ushahidi wao kuhusu kitita cha miti -shamba basi mimi sitohukumu kulingana na ushahidi wao."

Amma kuhusu Shi'ah wao wanadai yakwamba Maswahaba wote waliritadi (kuwacha dini) baada ya kifo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) isipokuwa watatu miongoni mwao. Na madai yao ya zaidi ni kuwa, kwa sababu wao ni makafiri, basi hapana mfano mzuri, kielelezo wala hadhi yoyote itakayoweza kuigwa kutoka kwa Maswahaba.

Amma kuhusu Khawaarij hawa wamepotoka kutoka kwenye dini na wakajitenga kutoka kwenye mwili mmoja wa Waislamu. Ni miongoni mwa itikadi zao kuthibitisha ukafiri juu ya 'Ali, wanawe wawili, Ibn 'Abbass, 'Uthmaan,Talha, 'Aaisha na Mu'aawiyah. Na yeyote anaewafanya hao kuwa ni shabaha yake na kuwatia kwenye ukafiri basi huyo hayupo juu ya njia ya Maswahaba.

Amma kuhusu Sufi, hawa wanadharau na kufanya maskhara kuhusu urathi wa Mitume (ilimu). Na wanawakanusha wapokezi wa Qur'an na Sunnah na kuwataja kwa sifa kama maiti. Kwani mmoja wa wazee wao alisema; "Wewe unachukuwa ilimu yako kutoka kwa maiti alie pokea kutoka kwa maiti (mwengine)', ambapo sisi tunachukuwa ilimu yetu kutoka kwenye 'Moyo wangu ukanihadithia mimi kutoka kwa Mola wangu (kuwa amesema kadhaa wa kadhaa)!"

Amma kuhusu Murjia', hawa wanadai eti imani ya wanafiki ni kama ile imani ya watangulizi wetu wa kwanza (Maswahaba)! Kwa ufupi, mapote haya yanajitahidi kuwabatilisha waliotushuhudilia Qur'an na Sunnah kwa macho yao (maswahaba) na kuupuuza ukweli wao, ambapo wao ndiwo wanaostahiki kupuuzwa.

Kutokamana na hayo imedhihirika yakwamba ufahamu wa Salaf ndiwo mfumo wa pote litakalo nusuriwa na pote la ushindi kuhusiana na ufahamu, kuilimika na kutumia ushahidi.

NENO LA BUSARA

"

Ikiwa hali imefikiya kiwango ambacho kila wakati Waislamu wawili wanapokhitilafiana kuhusu mas'ala fulani hususiana na kukatana wao kwa wao, basi hapatobaki hifadha wala Undugu baina ya Waislamu.

"

Sheikh 'Abdul-Muhsin al-'Abbaad